

ADHABU YA VIBOKO

Kama ilivyo kwa Wamarekani wengi, mimi sipati magazeti na nanunua kwa nadra. Habari zote nazipata kwa njia ya mtandano. Na jumapili iliyopita kabla ya ibada, nilikuwa nasoma vichwa vya habari fulani fulani, na vichwa vya habari kadhaa vilinivutia na ninapenda kuwashirikisha kidogo nilichosoma

Makala ya kwanza niliyoona imenivutia ilitoka Washington Post¹ na ilikuwa inazungumzia Temple shule ya wilaya huko Texas ambayo hivi karibuni imerudisha adhabu ya viboko kwa kura ya pamoja kutoka kwenye bodi ya shule. Tangu adhabu ya viboko irudishwe imeripotiwa kuwa kumekuwa na matokeo mazuri kuboreka kwa tabia za wanafunzi wa Temple. Na ubora huu umeonekana ingawa mtoto mmoja amepokea upendeleo wa pekee kwa maombi ya wazazi! Tishio dogo ni tosha kabisa kuwafanya wanafunzi watulie kitabia, kudhibiti ndimi zao, kuacha kupigana na kuwaheshimu walimu na viongozi zaidi. Ni ajabu kiasi gani! Mnairudisha adhabu ya viboko, na kila kitu kinabadilika kwa usiku mmoja! Kwa usiku mmoja!

Ukweli ni kwamba adhabu ya viboko imeondolewa karibu shule zote za wilaya leo kwa sababu walimu wachache na viongozi wangepindukia kiwango cha kuadhibu. Au baadhi ya watoto masikini walidhani wana thamani sana kucharazwa viboko na sasa ni watu wazima hivyo watajitalidi kuepa kifaa hiki bora cha nidhamu. Kifaa bora cha nidhamu, naishi kama uthibitisho.

Kwanza, linapokuja suala la adhabu lazima adhabu iwe endelevu. Moto mara zote huunguza, na tunajifunza hayo tangu utotoni. Wazazi na walimu wanatakiwa kuwa na mfumo endelevu wa adhabu kwa watoto na wanafunzi wao. Watoto wengi wanapata wakati mgumu sana katika kujua nini cha kufanya na kipi hawatakiwi kufanya kwa sababu wazazi na walimu wamewahi kukosa mfumo endelevu.

Pili, lazima tutambue kuwa si adhabu zote zinatakiwa kuwa hasi. Adhabu chanya inayofaa inaweza kusaidia, lakini hii ni kazi inayotakiwa kufanywa kwa hatua. Nimesikia kwamba ni sawa na kuvali vyuma kwenye meno. Kwa sababu jino lililochongoka likiwa na namna sahihi ya uweki mara kwa mara, huweza kuliweka vizuri jino. Walakini hatua hii haifanyi kwa usiku mmoja na ndiyo maana wakati fulani shuruti hulazimika kutumika. Yaani huhitaji miongo kupata matokeo!

Tatu, mtoa adhabu lazima awe ni kielozo kizuri tayari, Paulo alimwambia Timotheo, "mtu awaye yote asiudharau ujana wako, bali uwe kielelezo kwao waaminio, katika usemi na wmenendo na katika upendo na imani na usafi," 1 Timotheo 4:12. Endapo aliyewekwa kutoa adhabu hana mwenendo mzuri, basi mtu huyo hana haki ya kumwadhibu mtoto ye yote kwa analokuwa amefanya. Tendo hilo litavuruga pakubwa.

Nne, Watoa adhabu lazima watambue kuwa adhabu inayofaa ni ile inayokuwa tofauti tofauti. Kila mtoto yuko tofauti na mwingine. Ingawaje mfumo mzuri wa dahabu unaweza kusaidia kwa baadhi ya watoto, mfumo huo huo hauwezi kufaa kwa wote. Mimi ni mfano mkubwa wa hilo. Nilipokuwa shulenii, sikutaka king'ang'anizi fala! Sikujali kama nitapata yai mwishoni mwa juma la sita. Nilikuwa mwelewa mno kwamba kusoma kwa bidii ili uwe vizuri, wakati najua tuzo ni pulizo ilikuwa ni uwenda wazimu!!!!. Kila mtoto yuko tofauti, wengine wanachukulia mfumo mpya wa adhabu kama njama za kuhujumu haki ya kikatiba. Huu ujinga wa kuwacharaza viboko kwa kiwango kimoja ndicho kinachowarudisha nyuma watoto wetu leo. Wako tofauti na wanatakiwa kuchukuliwa hivyo na kuadhibiwa kitofauti. Si tu kwamba hili ni kweli katika suala la adhabu bali hata katika maeneo mengine. Tatizo ni kwamba, watu wazima wengi ni wavivu, na hawataki kuwa na muda wa kutosha na wanafunzi au mtoto ili kujua ni aina gani ya adhabu itasaidia kwa mtoto husika!

Tano, Watoa adhabu lazima waelewe kuwa adhabu wanayotoa inatoka katika moyo wa upendo. Mtoto lazima aelewewe kuwa unamwadhibu kwa sababu unampenda na unamjali. "Tena mmeyasahau yale maonyo, yasemayo nanyi kama kusema na wana " Mwanangu, usiyadharau marudia ya Bwana, wala usizimie moyo ukikemewa naye; Maana ye ye ambaye Bwana ampenda, humrudi, naye humpiga kila mwana amkubaliye," Wabrania 12:5-6

Sita, Adhabu nzuri inaleta matokeo katika akili. Tunamwadhibu mtoto kwa sababu anatukana, hatii, anavunja sheria, anagombana, n.k. Tunapotoa adhabu tunatakiwa tuelewe ni matokeo gani tunayotaka. Hatuadhibu, bali kurekebisha na kufinyanga. Tunasema kuwa sisi ni udongo na Mungu ni mfinyanzi, "Na chombo kile, alichokuwa akikifinyanga kilipoharibika mkononi mwake yule mfinyanzi, alikifanyiza tena kuwa chombo kingine, kama alivyoona vema yule mfinyanzi kukifanya. Ndipo Neno la Bwana likanijia, kusema, Ee nyumba ya Israeli, Je! Siwezi mimi kuwatendea vile vile kama mfinyanzi huyu alivyatenda? Angalieni, kama udongo ulivyo katika mkono ya mfinyanzi, ndivyo mlivyo ninyi katika mkono wangu, Ee nyumba ya Israeli," Yeremia 18:4-6. Jambo hili ni kweli kwa watoto na wanafunzi wetu!

Lazima tutambue kuwa watoto ni udongo ulio katika mikono yetu, kwa jinsi tunavyowaadhibu tutakuwa tunafinyanga kwa ajili ya maisha yao ya baadaye. Mithali 22:6 inasema, "Mlee mtoto katika njia impasayo, Naye hataiacha, hata atakapokuwa mzee." Na Mithali 13:24 inasema, "Yeye asiyetumia fimbo yake humchukia mwanawe, bali ye ye ampendaye humrudi mapema." Hili linatakiwa lifanyike kama Mungu alivyosema ili kupata matokeo!

Nimesikia wazazi wengi wakisema, "Nilimchapa mtoto wangu katika namna ambayo Biblia inasema, hebu mwangalie leo alivyo." Sawa, unaweza ukawa umemchapa mwanano, na shule inawezekana zimempa adhabu pia. Lakini swalii ni kwamba, adhabu uliyompa ilikuwa ya kumfunza na kumuadibisha kama mwenye hekima anavyofundisha? Je ilitokana na upendo kama marudia ya Mungu au ilitokana na kisirani na hasira (Waebriania 12:5-6)? Je! Ulizingatia

tofauti ya kila mtoto? Au uliweka kiwango tu kilichomfaa? Basi, usishangae kuona adhabu haijasaidia!

Kwa kuhitimisha, adhabu ya kweli lazima ichokonoe utu chanya ili isaidie. Na adhabu ya kweli huzingatia tofauti ya mtoto na mtoto. Na lazima ifanywe kwa upendo! Kwa lengo akilini!

Ninafurahi kwamba mfumo wa shule ya Temple umerudisha adhabu ya viboko. Siyo imfaayo kila mtoto. Lakini kwa wengine inafaa na kwa wengine kitisho tu kinatosha. Sasa hatutakiwi kumweka kila mtoto katika kiwango kimoja. Lakini kama shule na wazazi watashirikiana, shule itafahamu kuwa ni mtoto yupi anatakiwa adhabu ya kijeshi na mtoto yupi anahitaji fimbo. Kwa William, fimbo ni bomu! Anapenda na inasaida!

Walakini, ninakumbuka makuzi yangu na hirimu zangu. Na ninajua kuwa kama nisingekuwa ninachapwa kila siku, sikujisikia kupendwa. Lakini kwa upande wa dada yangu ilikuwa tofauti, alichokuwa anafanya baba ni kumwangalia tu. Kwa kumwangalia mara moja tu, kila kitu kilitatuliwa. Kwangu mimi, kutazamwa lilikuwa ni jaribu na mwanzo na siyo mwisho!

Kutazamwa kwangu mimi ilikuwa kama “huna mijeredi ya kunifukuzia hata unichape!” Kunitazama ilikuwa kama “we vipi, hebu tuone una nini.” Kunifokea ilikuwa kama “huwezi kunikataza.” Kuninyang’anya baiskeli yangu ilikuwa kama “nina miguu.” Lakini baada ya kuchapwa kwa mikanda mitatu minne hivi, “ ndiyo mkuu, nakusikiliza.” Nawaambieni, mkiondoa adhabu ya viboko kwa mtoto kama mimi, unakuwa umetengeneza vurugu!

Mungu aibariki Temple!